Wazazi na walezi wapendwa

Kama mulivio julishwa hapo awali, wazazi na walezi wa kila mtoto aliyejiandikisha katika shule ya serikali ya Victoria mwaka wa 2025 watapokea usaidizi wa matumizi ya shule mara moja wa $400.

Katika miezi ijayo, Idara ya Elimu itakutumia barua pepe 2 za mawasiliano kwa kila mtoto wako aliyejiandikisha katika shule za serikali ya Victoria.

Kufikia **Ijumaa tarehe 18 Oktoba 2024**, tafadhali hakikisha kwamba uandikishaji wa mtoto wako katika 2025 umekamilika na kwamba maelezo yako ya mawasiliano yamesasishwa.

Barua pepe 2 kutoka kwa Idara ya Elimu zita:
1. Thibitisha anwani yako ya barua pepe katikati mwezi ya Oktoba na mwishoni mwa Novemba.
2. Kukupa msimbo wako wa kipekee wa Bonasi ya Kutumia kwa shuguli za Shule ya $400 kufikia mwisho wa Novemba.

Iwapo hutapokea barua pepe ya uthibitisho kutoka kwa idara kufikia mwishoni mwa Novemba, tafadhali angalia folda zako za barua taka au taka na uwasiliane na WSSC ikihitajika.

Unaweza kusoma zaidi kuhusu Bonasi ya matumizi ya Shule kwenye tovuti ya Idara ya Elimu, na taarifa muhimu sasa zinapatikana katika lugha 14 tofauti.

Asanteni



Vern Hilditch
Mkuu wa Shule